This information is for promotional purposes only. Space considerations may require information to be omitted.
Always refer to the actual package for complete label language. This product may differ in content.

1630
FFN 04002

# AVAIL®

Mbolea ya Kuongeza Fosforasi

## AVAIL® KWA MBOLEA ZA FOSFETI YA CHEMBECHEMBE

Hupunguza kukwama kwa fosfeti

Kiambato Kinachotumika
30% w/w.......chumvi ya sodiamu nusu inayoyeyukia udongoni
70% w/w.......maji

Kemikali hii haitimizi vigezo vya hatari vilivyowekwa na Kiwango cha Mawasiliano ya Hatari cha OSHA cha 2012 (29 CFR 1910.1200).

### MAELEZO YA JUMLA

MBOLEA YA CHEMBECHEMBE ZA FOSFETI ZA AVAIL imeundwa ili kupuliziwa dawa kwenye mbolea za chembechembe za fosfeti (MAP, DAP na mbolea nyingine za chembechembe za fosfeti), kuondoa vyuma haribifu katika udongo unaokaribia chembechembe za mbolea, kupunguza kuganda kwa fosfeti na kufanya fosfeti ipatikane zaidi kwa mmea. AVAIL huongezeka upatikanaji wa fosfeti katka awamu zote za ukuaji wa mmea, ikiwa ni pamoja na kipindi cha ukuaji wa mapema ambacho ni muhimu kwa ajili ya kuongeza mavuno. AVAIL huyeyuka ndani ya maji, huzoea mchangani na haina sumu. Isipotatizwa, MBOLEA YA AVAIL KWA AJILI YA FOSFETI YA CHEMBECHEMBE huzuia kuganda kwa fosfeti na pia inaweza pia kutumiwa na mbolea za majira ya mapukutiko.

MBOLEA YA AVAIL KWA AJILI YA FOSFETI YA CHEMBECHEMBE NI KIAMBATO CHA CHAKULA KISICHO CHA MMEA CHAKULA NA HAIPENDEKEZWI KUTUMIKA BADALA YA MBOLEA.

### VIWANGO VYA MATUMIZI

Mbolea ya AVAIL iliyopakwa fosfeti inapaswa kutumika katika udongo katika namna sawa na mbolea ya fosfeti bila AVAIL.

KUMBUKA: Unapotumia AVAIL, ukitumia mbinu tofauti za kilimo mbinu kuliko za kawaida, vipande vya majaribio vinapaswa kutumika hadi mbinu hiyo mpya ithibitishwe kuwa ina ufanisi.

### AINA YA UDONGO NA MAZAO

AVAIL imeundwa ili kupunguza kuganda kwa mbolea ya fosfeti katika aina yoyote ya udongo na kutumiwa kwa mimea yoyote ambapo mbolea ya fosfeti imebainika kuwa muhimu kwa ukuaji wa mmea kwa mujibu wa mbinu bora za usimamizi.

### MAELEKEZO YA KUCHANGANYA

MBOLEA YA AVAIL KWA AJILI YA FOSFETI YA CHEMBECHEMBE inapaswa kunyunyizwa kwa usawa, wala si kumwagwa, kwenye mbolea za chembechembe ya fosfeti. Mbolea inapaswa kuwa kavu kabla ya kunyunyizia. Katika hali za baridi, kagua mnato wa MBOLEA YA AVAIL KWA AJILI YA FOSFETI YA CHEMBECHEMBE kabla ya kunyunyizia. Aina nyingi za vifaa vya kunyunyizia au kuchanganya hufanya kazi vizuri kutibu chembechembe hizi. Kuongeza uingizaji hewa na usafishaji bidhaa iliyonyunytizwa kutapunguza muda wa kukauka na kuongeza usambaaji wa AVAIL kwenye chembechembe za mbolea. Sehemu za ndani za vifaa za kuchanganya ambazo hazijafunikwa zinapaswa kuwa safi, kavu na bila kutu. Ruhusu mbolea nyevu kukakuka kabla ya kusambaza. AVAIL inapaswa kunyunyizwa kwenye mbolea ya fosfeti kabla ya kuchanganya na mbolea nyinginezo (km. nitrojeni au potasiamu).

Inapendekezwa kutumia pampu na viambatisho vya chuma cha "316" kisichoota kutu. Wakati vizuio vimetumiwa, vizuio vya "Gore-tex", "Teflon" au "Viton" vinahitajika

### VIWANGO VYA KUNYINYIZA

MBOLEA YA AVAIL KWA AJILI YA FOSFETI YA CHEMBECHEMBE imeundwa mahsusi kunyinyizwa kwa usawa kwenye mbolea ya fosfeti ya chembechembe kwa kiwango cha 0.25% au galoni ½ pipa la AVAIL kwa kila tani ya mbolea ya fosfeti ya chembechembe (lita 2.1 kwa tani).

### SIFA ZA KUZUIA KUUMBIKA KWA VIDONGE

MBOLEA YA AVAIL KWA AJILI YA FOSFETI YA CHEMBECHEMBE imethibitishwa kuzuia kuumbika kwa vidonge vya mbolea ambavyo wakati mwingine hutokea katika fosfeti ya chembechembe inapohifadhiwa kwenye mapipa.

### TAHADHARI YA MATUMIZI
### WEKA MBALI NA WATOTO
### USIIPUMUE WALA KUMEZA

Usitumie MBOLEA YA AVAIL KWA AJILI YA FOSFETI YA CHEMBECHEMBE katika mbolea ya fosfeti ya majimaji. USITUMIE kama mipako ya mbegu. Soma SDS na lebo kabla ya kutumia, ikijumuisha lakini si tu, "TAHADHARI YA MATUMIZI" na "Hakikisho/Vipimo vya Fidia". Kila wakati, vaa kinga sahihi ya kibinafsi na ufuate maelekezo ya matibabu na matumizi. Tumia kulingana na maelekezo yaliyo kwenye lebo.

Unapotumia AVAIL, daima vaa mavazi ya usalama kama vile vinyago na miwani ya usalama. Vaa mavazi yenye mikono mirefu, na suruali ndefu na utumie glavu za asili au za mpira. Tumia AVAIL latika maeneo yenye hewa ya kutosha. Kutokana na uwezekano wa kuwashwa macho na ngozi, epuka kuigusa Ikigusa macho au ngozi kimakosa, osha kwa maji mengi. Ikiwa kuwasha kutaendlea, pata usaidizi wa daktari. Inaweza kuwa hatari ikipimuliwa au kumezwa. Vifaa vitupu vinaweza kuwa na mabaki mbolea hii. Maonyo yote yaliyo kwenye lebo yanatumika kwa vifaa vitupu vya mbolea hii.

Usichafue njia za maji na mifereji ya uchafu inayovuja wakati wa kusafisha vifaa au kutupa taka, daima ukifuata sheria na kanuni husika za shirikisho, serikali ya kitaifa na mitaa sheria. Ondoa kabisa yaliyomo katika vifaa vya matumizi. Tupa ya vifaa vitupu katika mashimo ya kuzika taka, au kama ilivyobainisha na sheria husika. Usitumie upya vifaa vya mbolea. Fuata maonyo yote yaliyo kwenye lebo. Soma Karatasi ya Usalama wa Data kabla ya kutumia.

### HAKIKISHO

Verdesian Life Sciences U.S., LLC (VERDESIAN) inatoa hakikisho kwamba Bidhaa hii inalingana na maagizo yaliyowekwa kwenye lebo. Bidhaa hii ni mwafaka kwa lengo lililowekwa kwenye lebo ikitumika kulingana na maelekezo ya lebo na maagizo katika hali ya kawaida ya matumizi.

VERDESIAN HAIMLAZIMISHI, WALA KUMRUHUSU WAKALA YOYOTE, MWAKILISHI AU MTU MWINGINE KUTOA HAKIKISHO NYINGINEZO, MOJA KWA MOJA AU KWA NJIA ISIYO YA MOJA KWA MOJA, KISHERIA AU VINGINEVYO, KUHUSU HALI, UBORA, UWEZO KUUZWA AU UFAAFU WA VIUNGO KWA KUSUDI FULANI. Hakikisho la uwezo wa kuuzwa wala ufaafu kwa kusudi fulani, wa moja kwa moja au suio wa moja kwa moja, hauhusiki kwa matumizi ya Bidhaa hii kinyume na maagizo yaliyo kwenye lebo katika hali zisizo za kawaida au zisizotarajiwa na Muuzaji au VERDESIAN. Kipimo cha Fidia. Fidia ya kipekee ya hasara au uharibifu unaotokana na bidhaa hii (ikijumuisha madai yanayohusiana na mkataba, ukosefu wa umakinifu, dhima kali au nadharia nyingine za kisheria), hazitakiuka, kwa mujibu wa uamuzi wa VERDESIAN, mojawapo ya yafuatayo: (1) kubadilisha kiasi cha bidhaa kilichotumika; au (2) kurejeshewa pesa zinazolingana na bei iliyolipwa wakati wa kununua bidhaa hii; mradi utoaji wa VERDESIAN wa (1) au (2) unategemea kuarifiwa kwake mara moja kuhusu hasara au uharibifu huo kupitia maandishi. VERDESIAN haitawajibika kwa mnunuzi au mtu yoyote nyingine anayedai kwa, kupitia, au chini ya mnunuzi kwa hasara au uharibifu wowote mwingine unaotokana na au kuhusiana na bidhaa hii, ikijumuisha, lakini sio tu, uharibifu au hasara ya kifaida ya moja kwa moja, isiyo ya moja kwa moja, maalum, ya kiadhabu, kiuchumi, dhahiri au kubwa kwa mujibu wa mkataba huu, sheria au vinginevyo. VERDESIAN haikubali, wala haimruhusu mtu mwingine ruhusa ya kukubali kwa niaba yake, dhima nyingine yoyote inayohusiana na kuuza, kuhifadhi, kutumia au kushughulikia bidhaa hii kando na ilivyoelezwa waziwazi katika maelezo haya.

G

KWA AJILI YA MATUMIZI KWENYE MBOLEA YA FOSFETI YA CHEMBECHEMBE

KWA MATUMIZI YA KILIMO, NYASI NA MATUMIZI YA MAUA

SI BIDHAA YA CHAKULA MIMEA

Yaliyomo: Lita 946
Wiani: Kilo 1.29/Lita katika nyusi 24° C
Uzito wavu (1220.3 kg)
Kitambulisho cha: 20002634-000

VERDESIAN

Verdesian Life Sciences Europe Ltd
7 Rotherbrook Court, Bedford Road, Petersfield, GU32 3QG United Kingdom
**Huduma za Wateja:** +44 1730 720 100 / Technical@vlsci.com

Bidhaa hii imetengenezwa na:
**Verdesian Life Sciences, U.S., LLC**
1001 Winstead Drive, Suite 480, Cary, NC 27513. USA

**AVAIL** ni alama ya biashara iliyosajiliwa ya Verdesian Life Sciences. © 2015 Verdesian Life Sciences. Haki zote zimehifadhiwa.

SPECIMEN